

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
31 machi 2007**

Waliohudhuria

Abdallah Khatib

Elaine Baker

Juma Ali Salehe Jongo

Shukuru Hassan

Wageni

Mr Nyoni, AALOCOM

Prosper, AALOCOM

Dhumuni kuu la mkutano ni kuandika mchanganuo kwa jili ya kuandaa msafara wa baiskeli 2007. Elaine aliandika mchanganuo na kikao kiliupitia. Ilikubalika kuwa Prosper angeandika utangulizi kuhusu AALOCOM. Na Elaine atafuatilia CHABADA ili kupata utandulizi. Mabaadiliko kadhaa yalifanywa na nyongeza kwenye malengo ya msafara na mipango ya maandalizi.....

Jina la msafara lilijadiliwa. Prosper alipendekeza kuwepo jina jingine kuliko "msafara wa baiskeli" ila hakuwa na jina kwa haraka. Ilikubalika kufikiria jina zuri litakalotumika.

Tulifikiria kuhusu wafadhili na ITDP (kwa baiskeli za Califonia kama bahati nasibu na kwa mchango wa kifedha) kampuni ya Azam, (kwa ajili ya maji), Swala ya Mwenge, Parlay Chang'ombe (kwa uwezekano wa mchango wa baiskeli za mkono kwa walemavu kama bahati nasibu).

Prosper alisema kuwa anafahamu shirika jipya lisilo la kiserikali liitwalo TAISEFO ambalo lilipendelea kuandaa mafunzo ya ukarabati wa baiskeli. Alisema atawaunganisha na UWABA.

Elaine alisema kwamba UWABA imepokea barua kutok kwa katibu wa Waziri wa miundombinu. Barua inaunga mkono madhumuni ya UWABA, lakini akapendekeza kuwa tuonane na wadau wengine (wakala wa barabara-TANROADS, SUMATRA, Mamlaka ya usalama barabarani) kabla ya kuonanana na Waziri. Elaine alisema amepiga simu TANRODS Dar es Salaam mara kwa mara kufuatilia nakala za mpango wa barabara lakini mkurugenzi alikuwa nje ya ofisi. Prosper alisema kuwa ofisi za SUMATRA ziko mjini katika jengo la PPF tower. Ilikubalika kuendelea kufuatilia TANROADS na kaomba miadi na SUMATRA.

Juma aliripoti kuwa alifuatilia na akapata jibu kutoka idara ya usalama barabarani na akapata jibu tawi la Dar es Salaam la polisi kuomba kumbukumbu za ajali za baiskeli. Kumbukumbu katika barua zinaonesha kama ifuatavyo:

Mwaka	Idadi ya ajali	Idadi ya vifo	Majeruhi	Idadi ya baiskeli
2005	321	17	300	324
2006	314	30	306	314

Iikubalika kwamba kumbukumbu hizi zitakuwa muhimu katika utoaji wa mada. Juma alisema kwamba mtu aliyeongea nae katika ofisi hii alingalia tovuti ya UWABA na kuvutiwa

Iikubalika kwamba AALOCOM na UWABA wangakuta kwa wiki mbili tarehe 14/4 saa 4 asubuhi Masai Baa kufanya mapitio ya mchanganuo wa msafara wa baiskeli.